# BRIGHT VISION SERIES
# DARASA LA NANE - MWAKA - 2023
SASON 003
# KISWAHILI : LUGHA

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

I) JINA LAKO II) JINA LA SHULE YAKO MUDA: SAA 1 DAK. 40

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Mechi __1__ timu ya shujaa na hodari __2__ sana kijijini. Uwanjani __3__ mashabiki __4__ kuzishangilia timu zao. Wachezaji nao walijikaza __5__ almradi wazipatie timu zao ushindi. __6__ cha mwisho __7__ timu ya hodari ilikuwa mbele kwa bao moja kwa __8__. Wachezaji wa shujaa walielewa kuwa __9__ waliwapongeza wenzao kwa ushindi huo na kuwaahidi mashabiki wao kuwa wangecheza vizuri zaidi katika mechi na ambazo zingetungwa.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. dhidi ya | B. baina ya | C. katikati ya | D. juu ya |
| 2. | A. ilitia fora | B. ilipiga mbiu | C. ilikuła mwata | D. ilipiga chaka |
| 3. | A. wote kulijaa | B. wote palija | C. mote kulijaa | D. pote palijaa |
| 4. | A. waliyokuja | B. walikokuja | C. waliokuja | D. waliyekuja |
| 5. | A. kisabuni | B. kikondo | C. kijogoo | D. kipopo |
| 6. | A. firimbi | B. kipenga | C. kipuli | D. kengele |
| 7. | A. ilipolia | B. ulipolia | C. kilicholia | D. kilipolia |
| 8. | A. mawili | B. tatu | C. nunge | D. mbili |

9. A. asiyekubali kushindwa si mshindani
   B. mbio za sakafuni huishia ukingoni
   C. mtaka cha mvunguni sharti ainame
   D. asiye kujua hakuthamini

Sekta ya viwandani ni muhimu sana __10__ haijapewa umuhimu __11__ humu nchini. Viwanda vyetu vikiimarishwa vijana wetu __12__ ajira hivyo basi kukabiliana na makali ya ukosefu __13__ kazi. Jukumu la kuanzisha viwanda sio tu la serikali __14__ ni wajibu wa __15__ wa kibinafsi.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. lau | B. japo | C. maadamu | D. wala |
| 11. | A. vifaavyo | B. ifaayo | C. ufuavyo | D. ufaao |
| 12. | A. wangapata | B. wakapata | C. watapata | D. wanapata |
| 13. | A. wa | B. ya | C. kwa | D. na |
| 14. | A. mbali | B. bali pia | C. ila pia | D. ilhali |
| 15. | A. walowezi | B. mahairi | C. wazalendo | D. wawekezaji |

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

16. Chagua kundi lenye vielezi pekee.
   A. Gani, yule, vyenyewe
   B. Kumbe, ala, salaale
   C. Juu ya, chini ya, kwenye
   D. Sana, mtoni, juzi

17. ***Andika wingi wa sentensi ifuatayo.***
   Dobi aliusifu upishi wa dada yangu.
   A. Dobi waliusifu upishi wa dada zetu
   B. Madobi waliyosifu mapishi ya dada zetu
   C. Dobi waliyasifu mapishi ya dada zetu
   D. Madobi waliusifu upishi wa dada zetu

18. Msemo "**shangazi ametuacha mkono**" una maana kuwa
   A. ameondoka
   B. ametupongeza
   C. amefariki
   D. ameacha kutusaidia

19. Kutokana na kitenzi cheka tunapata sifa.
   A. mcheshi
   B. ucheshi
   C. kicheko
   D. chekesha

20. Mvua ingenyesha vizuri tungepata mavuno mengi. Maana ya sentensi hii ni kuwa
   A. Mvua ilinyesha vizuri japo hatukupata mavuno mengi
   B. Mvua ikinyesha vizuri tutapata mavuno mengi



LIVEWORKSHEETS

C. mvua haikunyesha vizuri hatukupata mavuno mengi
D. mvua ilinyesha vizuri tukapata mavuno mengi

21. Sehemu ya bei kamili inayotolewa mwanzoni ili kukifunga kitu huitwaje?
A. Arbuni B. Kiinua mgongo
C. Ujira D. Kiokozi

22. Kata ni eneo la utawala kata pia ni
A. mahali pa kuchotea na kunywea maji
B. kosa kukubaliana na jambo
C. mzigo uliobebwa kichwani au begani
D. kitambaa cha kufungia jeraha

23. ***Andika katika hali ya ukubwa.***
Mbwa alibweka alipomwona ng'ombe mkubwa.
A. Kijibwa kilibweka kilipokiona kigombe kikubwa
B. Jibwa lilibweka alipomwona gombe mkubwa
C. jibwa lilibweka lilipoliona gombe kubwa
D. mbwa lilibweka lilipomwona gombe kubwa

24. ***Tegua kitendawili kifuatacho.***
Hachoki wala halemewi kubeba.
A. meli B. ndovu
C. ardhi D. mauti

25. Neno lipi lina silabi yenye sauti changamano?
A. Sherehe B. Fadhaa
C. Mkono D. Mbweha

26. ***Bainisha matumizi ya kwa katika sentensi.***
Melisa alimwendea mwalimu wake kwa ushauri
A. Kuonyesha kusudi la kufanya jambo
B. Kuonyesha uhusiano wa mtu na mahali
C. Kuonyesha jinsi ya kutenda jambo
D. Kuonyesha sehemu ya kitu kizima

27. Baridi ni kwa barafu ilhali chungu ni kwa
A. pilipili B. shubiri
C. ghadhabu D. chakula

28. Kipande cha pili cha mshororo katika shairi huitwaje?
A. Mloto B. Tathnia
C. Utao D. Mwandamizi

29. Chagua jibu linaloonyesha nomino ya jamii.
A. Halati B. Fungu
C. Marashi D. Wema

30. Ni methali gani iliyo na maana sawa na hii?
Zimwi likujualo halikuli likakumaliza
A. Ibilisi wa mtu ni mtu
B. Damu ya kunguni balaa
C. Asiyekujua hakuthamini
D. Damu ni nzito kuliko maji

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Ili kukomesha unyanyasaji wa kujinsia hatua kadhaa hazina budi kuchukuliwa. Hatua kuu kabisa kati ya hizi ni utoaji wa elimu kuhusu usawa wa kijinsia na madhara ya unyanyasaji wa kijinisia. Kupitia elimu, kila mmoja atazijua haki zake na za wengine. Raia walioelimika huelewa bayana kuwa unyanyasaji wa kijinsia ni jambo ambalo tumelipa kisogo katika ulimwengu wa sasa..

Mbali na elimu, ni vyema pawe na sheria mwafaka zinazolinda jinsia zote. Sheria iweke wazi kuwa mwanaume asimdhulumu mwanamke wala huyo mwanamke naye asimkandamize mwanamume kwa vyovyote vile. Wanaokiuka sheria hizo kwa kujitia upofu wa kutoelewa nao wakabiliwe vikali kwa kufunguliwa mashtaka. Aidha, sheria hizi ziwekwe wazi ili kila mmoja apate kuzijua.

Familia ni asasi muhimu sana katika jamii. Unyanyasaji wa kijinsia unafaa kukabiliwa pale nyumbani. Mzazi awafunze watoto tangu wakiwa wachanga kuwa hawapaswi kubaguana kwa msingi wa kijinsia, isitoshe, awe tayari kuwakosoa na kuwaelekeza iwapo wataonyesha dalili za kuuasi mkondo ufaao wa malezi. Isitoshe, awe tayari kuwakosoa na kuwaelekeza iwapo wataonyesha dalili za kuuasi mkando ufaao wa malezi. Tuzingatie nasaha ya wahenga kuwa **samaki mkunje angali mbichi**." Watoto wakifunzwa kuheshimiana tangu wakiwa wadogo, watazingatia usawa wa kijinsia hata wakikomaa. Mzazi naye awe na budi kuwa kielelezo bora kwa kupinga unyanyasaji wa kijinsia kwa matendo na maneno.

Mtoto akitoka nyumbani hufika shuleni ambapo hujiunga na jamii pana zaidi. Mwalimu mshikadau wa elimu na ahata wanafunzi wenye hawana budi kushikana mikono katika kukomesha unyanyasaji wa kijinsia. Maendeleo haya ndiyo yatakayomwongoza mwanafunzi hata baada ya kuhitimisha elimu yake shuleni.

Vijana kwa jumla wana uwezo mkubwa wa kuwahamasisha wenzao kuandama hulka zifaazo. Wanaweza kufanya hivi kupitia sanaa kama vile muziki, uchoraji, uigizaji au hata vikao vya mazungumzo. Kwa njia hii watafikia jamii pana zaidi na kijinsia.

Viongozo wa kijamii huwa na mchango katika jamii. Wao ndio hutoa mwelekeo kuhusu mila na desturi na hata utatuzi wa migogoro katika jamii wanazozisimamia. Hawa wakijitolea kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, wanajamii wengine watazingatia maelekezo ya jinsi maji yafuatavyo mkondo. Viongozi wa kidini aidha wakiwaelekeza waumini kwa njia iliyo bora juhudi hizo zitaleta manufaa makubwa.



LIVEWORKSHEETS

Mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa katika mstari wa mbele kupigana na nyanyasaji wa kijinsia. Tumeshuhudia taarifa katika vyombo vya habari ambapo mashirika hayo yamewaokoa wahasiriwa hao na kuwachukulia hatua wakandamizaji. Sote tunapaswa kuziunga mkono jitihada za mashirika hayo.

Vyombo vya dola kama vile polisi vinapazwa kuwajibika ipasavyo ili kukomesha unyanyasaji wa kijinsia. Visa hivi vikiripotiwa, waliotwikwa jukumu la kuwakabili wakandamizaji wasiendelee kupakata mikono. Wachukue hatua zifaazo mapema kwani chelewa chelewa utapata mwana si wako. Hatua zisipochukuliwa mapema huenda wahasiriwa wakaendelea kuathirika zaidi huku watekelezaji wakiongezeka na kuwa na kiburi.Maelekezo haya yakifuatwa hatua kwa hatua tutakomesha unyanyasaji wa kijinsia kabisa.

31. Chagua jibu sahihi
A. unyanyasaji wa kijinsia umeenea kotekote
B. si rahisi kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia
C. wote wakipata maarifa yafaayo unyanyasaji wa kijinisia utakoma
D. elimu ndiyo njia pekee ya kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia

32. Ni vyema kuwa na sheria ili
A. dhuluma dhidi ya wanawake zikomeshwe
B. maslahi ya wote yashugulikiwe ipasavyo
C. wanaume katili waogope vitendo vyao
D. wanajamii waache kujitia upofu

33. Familia nimuhimu kwa sababu
A. unyanyasaji mara nyingi huanzia nyumbani
B. wazazi ndio walimu bora zaidi katika jamii
C. mtoto huweza kutangamana na watu wengi zaidi
D. ni kiini cha elimu ya mtoto yeyote

34. Methali "**samaki mkunje angali mbichi**" imetumika kuonyesha kuwa,
A. mtoto akifunzwa kuwajali wengine mapema hatakiuka hali za wenzake
B. mienendo ya wazazi ikiwa mizuri, watoto watawaiga na kuwa waadhifa
C. watoto wasipoonyesha dalili mbaya mapema, kuna uwezekano wa kupotoka baadaye
D. mtoto akielewa kunakoendelezwa unyanyasaji, atajifunza madhara ya jambo hilo

35. Elimu anayopata mtoto shuleni
A. hudhamiriwa kumpatia kazi baadaye
B. huwa mwongozo katika maisha yake ya baadaye
C. humsaidia kuitambua jamii yake baadaye
D. huonyesha yatakayotokea baadaye

36. Vijana
A. ndio wanaowakandamiza wenzao zaidi
B. hawahusiki katika unyanyasaji wa kijinsia
C. ni msingi wa kuiadilisha jamii pana
D. wamekithiri katika unyanyasaji

37. Mchango wa viongozi wa kijamii ni muhimu kwa sababu
A. wanaheshimika kote kwa umri wao mpevu
B. wanatarajiwa kuwaelekeza waumini ipasavyo
C. wao ndio hutoa adhabu kwa wakiuki sheria
D. wao ndio hutoa mwongozo wa kuiendesha jamii

38. Mashirika yasiyo ya kiserikali
A. huwasaidia wahasiriwa kuzitetea haki zao
B. huwahukumu wanaondeleza unyanyasaji wa kijinsia
C. wanajamii wote wamepakata mikono huku maovu yakishamiri
D. yanalaumiwa kwa kutochukua hatua zifaazo

39. Kulingana na aya ya mwisho
A. huenda kuna wale wasiowajibika katika majukumu yao
B. vyombo vya dola vinaendeleza unyanyazaji wa kijinisia
C. wanajamii wote wamepakata mikono huku maovu ya kishamiri
D. hakuna hatua zilizochukuliwa kufikia hapa

40. Maneno **tumelipa kisogo** yana maana kuwa
A. tumelipuuza B. limepitwa na wakati
C. limesahaulika D. tumelifumbia macho

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Mara tu faraja alipotia mguu katika shule ya upili ya Songambele, kila mwanafunzi alifahamu kuwa asili yake ilikuwa ya kichochole. Mavazi yake yalichakaa na viatu vyake vilichoka kutiwa miguuni mwa mvaaji. Vilitangaza kwa kishindo kikubwa. Japo havikunena kuwa kweli. Faraja ni mkata.

Kuna wanafunzi waliombezi na **kumchezea shere**. Wengine walimwona kama kinyangarika duni kisichofaa kuwa miongoni mwao.Hata hivyo, wapo waliomwona kama dada yao na kushirikiana naye kwa udugu mkubwa. Waliomdharau hawakufahamu kuwa **aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa kumbi**.

Wakati ulivyozidi kuusukuma mbele muhula ndivyo faraja naye alivyokakawana na masomo yake. Alijisabilia kwa ukucha na meno na matokeo yake yalionyesha kuwa yeye ndiye aliyeongoza



LIVEWORKSHEETS

darasani. Mihula yote mitatu ya kidato cha kwanza aliongoza yeye nao walimu wakawa wakimhimiza kutolegeza kamba. Wenzake waliomdharau walijibu kumpiku lakini wapi! Ilikuwa kama garimoshi ambalo pindi ling'oapo nanga halisiti mwendo mpaka kidato cha pili.

Faraja alijishindia mzo wa zawadi ambazo zilimpa mshawasha mkubwa wa kudurusu vitabu vyake mara kwa mara. Sasa alijiamini sana. Palipoandaliwa mashindano na shule nyingine daima aliongoza tena kwa mara nyingine. Sauti ya faraja ilisikika tu kwenye mashindano ya aina hii katika mazingira mengine. Isingejulikana kuwa alikuwa msemaji stadi mwenye ulimi unaotema lugha fasaha.

Kufikia kidato cha nne, Faraja hakuwa ameadhibiwa wala kupatishana matata na yeyote. Kila mmoja alipendezwa na hulka yake ya heshima, unyenyekevu na kutoa ushauri kwa wenzake tayari alikuwa kaasis chama cha kutoa huduma za ushauri wa aina mbali mbali kwa vijana shuleni. Ushauri huo ulihusu heshima na nidhamu shuleni, madhara ya dawa za kulevya hasa kwa vijana na hatari iliyopo katika kushiriki mapenzi ya kiholela. Alikuwa sasa kivutio cha wote shuleni humo. Hata waliomchukia kwa kumtazama tu alipoingia shuleni Songambele walimwenzi kama mboni ya macho yao.

Matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne yalipotangazwa, faraja alikuwa kapita vizuri. Aliweka rekodi mpya ya kitaifa. Darasa lake nalo lilifanya vizuri. Siku chache baada ya matokeo hayo, alipita mzungu mmoja kwa nia ya kushauriana wito wa serikali wa elimu kwa wote bila ubaguzi ulikuwa njozi ili iliyopotea. Mama yule aliona kuwa njia ya pekee ya kumtafutia ufadhili wa kumtuma ng'ambo kusomea udaktari.

Huu ulikuwa mwanzo wa mkoko kualika mama kwani waliomfadhili walikuwa na mpango wa kuanzisha shirika lenye kutetea haki za watoto wa kike nchini mwao. Shirika hili lilitaka usimamizi wake. Kuongozwa na mwenyeji aliyesomea udaktari na masuala ya haki za watoto hasa wa kike. Faraja alikuwa mwananchi wa kwanza kuenda kusomea haya. Siku ile alipoabiri ndege kuenda ulaya, hakujua kuwa mambo mapya yalikuwa yakimsubiri yeye nyumbani baada ya kuhitimu ila kuja kuyaendeleza.

41. Mara tu faraja alipojiunga na shule ya upili ya Songambele
   A. alijitangazia hali yake ya uchochole uliokithiri
   B. waliomwona walimdharau kutokana na hali yake
   C. alipokelewa kwa hisia mseto shuleni humo
   D. walimu kwa wanafunzi walimdharau kwa hali yake duni

42. Faraja alifanya vyema shuleni kutokana na
   A. zawadi, himizo na kero la wenziwe
   B. ari, shime na tuzo alizokabidhiwa
   C. nia ya kuupiga kumbo uchochole wake
   D. bidii, shime za wanafunzi na ushindani aliopata

43. Faraja analinganishwa na garimoshi kutokana na
   A. kujikokota kutekeleza shughuli ipasavyo
   B. kujisaga sana ili kutimiza ndoto zake
   C. kupongezwa na walimu wote shuleni
   D. kuendelea mbele bila kurudi chini masomoni

44. Bila shaka kujiamini kwa faraja ni zao la
   A. ushindi uliopata   B. kupendwa na walimu
   C. jitihada zake   D. ulegevu wa wenzake

45. Kipawa cha faraja kilidhihirika katika
   A. uandishi bora
   B. ulumbi
   C. heshima na unyenyekevu
   D. michezo hasa riadha

46. Wazo kuu analotoa mwandishi katika aya ya tano ni kuwa
   A. vijana hujiingiza katika maovu ya mapenzi na mihadarati
   B. mtu akitenda vyema hupendwa hata na maadui zake
   C. si vyema kuwawekea kinyongo wale wanatuehukia
   D. nasaha zilizo na vijana zinaweza kuwabadilisha wenzao

47. Waliomchukia Faraja kwa kumwona siku ya kwanza watazinduliwa kwa methali gani?
   A. Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake
   B. Mambo ni kangaja huenda yakaja
   C. Asiyekujua hakuthamini
   D. Kikulacho ki nguoni mwako

48. Kwa mujibu wa kifungu ni kweli kuwa
   A. serikali haikuwa na mawazo mazuri kuhusu elimu
   B. wasichana ndio waliopendelewa kwa kupewa udhamini
   C. waliomdhamini Faraja ni wenyeji wa nchi yake
   D. matokeo bora darasani yalitokana na mwongozo mzuri

49. Faraja alikuwa na nafasi bora ya kuajiriwa na shirika lililoanzishwa na wafadhili wake kwa kuwa alikuwa
   A. mtu wa kwanza kusomea taaluma husika
   B. na mlahaka mwema na wahisani wake
   C. wa kwanza kutimiza masharti yaliyohitajika
   D. mwenye heshima bidii na kufuzu vyema

50. Maana ya **walimchezea shere** ni kuwa
   A. walimdhihaki   B. walimbeza
   C. walimdharau   D. walimtwaza



LIVEWORKSHEETS